

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

**JEDWALI LA MAJIBU YA WIZARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA
NDOGO**

MACHI, 2025

TANGAZO LA SERIKALI	JINA LA SHERIA NDOGO	YALIYOBAINIKA	MAONI	UTEKELEZAJI/UFAFANUZI	
1. (Tangazo la Serikali Na. 809 la mwaka 2024)	Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote (Zimetengeneza chini ya kifungu cha 35)	1. Kanuni ya 13 (3) inazipa jukumu Mamlaka za utambuzi kushirikisha wadau kwa ajili ya orodha ya watu wasio na uwezo <u>Tatizo</u> a) Kanuni inazitaka mamlaka kushirikisha wadau ilhali jukumu hilo linatekelezwa na mamlaka za utambuzi kwa mujibu wa kanuni na taratibu zinazosimamiwa na Wizara nyingine zinazohusika. Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Wizara ambazo Mamlaka za utambuzi zipo chini yake. b) Kanuni haijaweka utaratibu wake mahsusi wa kutambua taarifa za watu wasio na uwezo. Hali hii inaweza kusababisha Wizara kutokuwa na taarifa muhimu hivyo kukwamisha utekelezaji wa lengo la sheria mama.	Kanuni ziweke utaratibu wa namna ya kuwatambua watu wasio na uwezo utakaoratibiwa na Wizara moja kwa moja kwa kushirikiana na Mamlaka za utambuzi zinazotambuliwa na Kanuni hizi.	Maoni yamezingatiwa. Kanuni kuu imefanyiwa marekebisho kupitia Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa wote za mwaka 2025, TS. Na. 192 la tarehe 21/03/2025 kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:	
				“Utaratibu wa utambuzi wa watu wasio na uwezo	13.-(1) Kwa madhumuni ya ujumuishaji wa watu wasio na uwezo katika mfumo wa bima ya afya, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za utambuzi itaandaa mwongozo utakaobainisha vigezo vya utambuzi wa watu wasio na uwezo. (2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kanuni hii, Wizara itaziomba mamlaka za utambuzi wa watu wasio na uwezo kutambua na kuwasilisha kwake, katika muda utakaobainishwa, taarifa zinazohusiana na watu wasio na uwezo. (3) Mamlaka za utambuzi zitafanya utambuzi wa watu wasio na uwezo kwa kuzingatia vigezo vilivyobainishwa katika mwongozo wa utambuzi wa watu wasio na

uwezo na kuwasilisha taarifa kwa Wizara.

(4) Wizara mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mamlaka za utambuzi chini ya kanuni ndogo ya (3), itajumuisha orodha ya watu wasio na uwezo waliotambuliwa katika kanzidata ya watu wasio na uwezo kwa ajili ya kugharamiwa bima ya afya.

(5) Wizara inaweza, pale itakapohitajika na kwa namna itakayoona inafaa, kufanya uhakiki wa taarifa za watu wasio na uwezo zilizojumuishwa katika orodha ya watu wasio na uwezo.”

Ufafanuzi: kwa kuwa vigezo vya utambuzi vitakuwa vinabadilika mara kwa mara kulingana na hali ya uchumi wa nchi, kukua au kushuka kwa vipato vya wananchi, au shughuli za uzalishaji ndani ya nchi na sababu zingine ambazo zinaweza kujitokeza, vigezo vya kuwatambua watu wasio na uwezo vimependekezwa kuwekwa katika Mwongozo utakaoandaliwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya afya. Lengo ni kuepuka kufanya marekebisho ya Kanuni mara kwa mara.

2. **Kanuni ya 15(3)** inahusu uendeshaji

Kanuni ya 2

Maoni yamezingatiwa. Kanuni kuu

		wa kila siku wa mfuko utakaosimamiwa na Skimu ya Bima ya Afya ya Umma <u>Tatizo</u> Mamlaka ya usimamizi wa uendeshaji wa mfuko pia ina jukumu la kutoa huduma ya kugharamia bima za afya kwa watu wasio na uwezo. Majukumu haya yakifanyika kwa pamoja yanaondoa dhana ya uwajibikaji wa Skimu ya Bima ya Afya ya Umma. Utaratibu wa usimamizi wa mfuko uliowekwa na kanuni ni kinyume matakwa ya kifungu cha 25(4) cha sheria mama kinachomtaka Waziri kuweka utaratibu wa usimamizi bora wa mfuko.	ifanyiwe marekebisho kwa kurekebisha tafsiri ya neno “Mfuko” ili kuonesha ni akaunti na si mfuko unaoanzishwa kama taasisi.	imefanyiwa marekebisho kupitia Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa wote za mwaka 2025, TS. Na. 192 la tarehe 21/03/2025 kwa kuongeza katika Kanuni ya 2, tafsiri ya ifuatayo: “Mfuko” maana yake ni akaunti ya fedha za kugharamia watu wasio na uwezo kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 25 cha Sheria.”
		3. Kanuni ya 18 iinahusu udhibiti wa huduma za bima ya afya na kanzidata ya vituo vya huduma za afya. <u>Tatizo</u> a) Kanuni ya 18(1) (b) imetaja ngazi za kituo cha kutolea huduma za afya kama mojawapo ya taarifa itakayotunzwa na mamlaka kwenye kanzidata, pasipo kuweka tafsiri ya neno “ngazi”.	Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kurejea Mwongozo wa Utoaji Huduma wa Vituo vya Afya, 2017.	Maoni yamezingatiwa. Kanuni kuu imefanyiwa marekebisho kupitia Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa wote za mwaka 2025, TS. Na. 192 la tarehe 21/03/2025 kama ifuatavyo: 18.-(1) Mamlaka itatunza kanzidata ya vituo vya huduma za afya vilivyoingia Mkataba na skimu za bima ya afya ikijumuisha taarifa zifuatazo: (c) ngazi ya kituo cha kutolea huduma za afya kwa kuzingatia miongozo ya utoaji

		Hali hii inaweza kusababisha kubaki na fasiri ya mazoea na kuondoa uwezekano wa aina zingine za vituo kutambulika ngazi zake na hivyo kushindwa kushiriki kuwahudumia watanzania.		huduma kwa vituo vya kutolea huduma za afya.
		4. Kanuni ya 24 (1)(a) inainisha sababu zinazoweza kusababisha ukomo wa uanachama katika skimu ya Bima ya Afya. <u>Tatizo</u> Kanuni inaweka ukomo wa mwanachama ambaye ni mwajiriwa wa sekta ya umma kupata huduma ya skimu kutokana na kutochangia ndani ya miezi mitatu mfululizo. Kanuni haijazingatia wajibu aliopewa mwajiri katika sekta ya Umma chini ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura ya 395.	Kanuni iweka utaratibu wa kumjulisha mwajiriwa kabla ya kusitisha huduma pale ambapo mwajiri ameshindwa kuwasilisha michango.	Maoni yamezingatiwa. Kanuni kuu imefanyiwa marekebisho kupitia Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa wote za mwaka 2025, TS. Na. 192 la tarehe 21/03/2025 kwa kuongeza kanuni ndogo ifuatayo;- “(2) Skimu ya bima ya afya itamjulisha mwanachama kwa maandishi, kuhusu uanachama wake kufikia ukomo kwa sababu za kushindwa kuchangia, mwezi mmoja kabla ya kufikia ukomo.”
		5. Kanuni ya 30 (1) inaeleza kuhusu kuwa huduma zinazopatikana kwenye kitita cha mafao ya huduma muhimu zitakuwa kama zilivyobainishwa kwenye sheria mama.	Wizara ikamilishe haraka mchakato na wadau ili kujumuisha huduma za kitita cha mafao ya	Maoni yamepokelewa. Wizara inaendelea kukamilisha mchakato wa kuandaa vitita vya mafao, na baada ya hatua hiyo Kanuni itafanyiwa marekebisho na kujumuisha huduma za vitita vya mafao.

		<u>Tatizo</u> Kanuni imefanya rejea ya huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu zilizotajwa chini ya Jedwali A la sheria. Kanuni haijatoa ufafanuzi wa kina kama ilivyoelekezwa katika Jedwali A kuhusu huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu zitatolewa. Kutokuainisha aina za huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu ni kukwamisha utekelezaji wa masharti sheria mama.	huduma muhimu katika Kanuni.	Hadi sasa wadau walioshirikishwa ni: Waganga wafawidhi wa hospitali za rufaa za Mikoa, hospitali za wilaya, TAMISEMI na Makatibu Wakuu. Wadau waliobaki ambao Wizara inatarajia kuwafikia ni pamoja na:- Sekta Binafsi, Taasisi za kidini, vyama vya kitaaluma pamoja na vyama vya wafanyakazi. Baada ya kukamilika, vitita vitawasilishwa TIRA kwa ajili ya upekuzi/uhakiki ili kuona kama vinaendana na uhalisia wa soko.
		6. Kanuni ya 35 inahusu kitita cha huduma za ziada. <u>Tatizo</u> Huduma za kwenye kitita cha huduma za ziada haijafafanuliwa katika Kanuni kama ilivyoelekezwa na Kifungu cha 35 (b) cha sheria mama kinachompa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazoainisha kitita cha mafao, muda, masharti au wigo wa kitita cha mafao.	Kanuni iweke tafsiri ya vitita vya Bima ya Afya	Maoni yamepokelewa. Aidha, Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura 161 imeweka tafsiri ya vitita vya mafao. Hivyo, kwa kuwa Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote zinasomwa pamoja na Sheria, inapendekezwa Kanuni kubaki kama zilivyo.
		7. Kanuni ya 36 (3) kimeelekeza kituo kutoa sababu za msingi na madai yanaweza kukubaliwa au kukataliwa na skimu, Kanuni ya 37 (2) imeipa skimu mamlaka ya	Wizara ione namna nzuri ya kulipa kufidia kwa kituo cha afya kutokana na	Maoni yamezingatiwa. Kanuni kuu imefanyiwa marekebisho kupitia Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa wote za mwaka 2025, TS. Na. 192 la tarehe 21/03/2025 kwa kufuta kanuni ya 37(2)

		kuongeza muda wa siku 15 kwa kutoa taarifa ya kusudio. <u>Tatizo</u> a) Kanuni zote kwa pamoja hazitoi fursa sawa kati ya mtoa huduma na skimu ya bima ya Afya katika kushughulikia masuala baina yao, skimu imepewa nguvu ilihali washirika hawana uwezo huo. b) Kanuni ya 36(3) inaeleza madai ya kituo yakichelewa, skimu inaweza kukubali au kuyakataa madai hayo, lakini haisemi kituo kina nafasi gani kukubali au kukataa kusudio la skimu kuongeza siku 15 baada ya siku 60. Ikizingatiwa hii inafanya kuwa na siku 75 za malipo, wakati asilimia kubwa ya credit facilities kwenye soko la bidhaa ni siku 60.	ucheleweshaji wa malipo uliosababishwa na Skimu ya bima ya Afya. Pia Wizara iangalie upya muda wa kushughulikia madai hayo kwa ujumla kwani muda uliotajwa na kanuni hii kiuhalisia ni mwingi.	inayoweka muda wa nyongeza wa siku 15. Hivyo, kwa sasa muda wa kukamilishwa kwa malipo ni siku sitini (60). Aidha, kuhusu suala la fidia kwa kituo, kwa sasa Kanuni 37 (3) imebainisha sharti kwa skimu itakayochelewesha malipo, kukilipa kituo husika malipo hayo pamoja na faini ya asilimia tano (5%) kama fidia ya ucheleweshaji. Hivyo, inapendekezwa Kanuni ibaki kama ilivyo katika eneo la ulipaji wa fidia.
		8. Kanuni hizi zimetungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa masharti ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, 2023. <u>Tatizo</u> a) Kanuni haioneshi mambo muhimu yaliyoelekezwa na sheria mama kama vile Viwango vya uchangiaji kwa ajili ya sekta	Marekebisho yafanyike kwa kuweka mambo muhimu yote ambayo yametambuliwa na Sheria mama kuwa yatafafanuliwa na kanuni hizi.	Maoni yamepokelewa. Aidha, kwa sasa masuala ambayo hayajatungiwa Kanuni ni yale ambayo maandalizi yake hayajakamilika au ambayo hayahitajiki kwa sasa. Hivyo, masuala hayo yatakapokamilika au kuhitajika Kanuni zinaweza kufanyiwa marekebisho au Kanuni mpya kutungwa ili kujumuisha masuala hayo.

		ya umma, sekta rasmi binafsi na sekta isiyo rasmi; Kanuni inaelekeza masuala mbalimbali kutolewa ufafanuzi katika miongozo badala ya kuekwa katika Kanuni kama ilivyoelekezwa na sheria mama.		Hivyo, inapendekezwa, Kanuni kubaki kama ilivyo.
--	--	---	--	---